TARI-
MLINGANO

# KILIMO BORA CHA

# ZAO LA MKONGE




Kimetayarishwa na

Kituo cha Utafiti wa Kilimo, TARI-Mlingano

S.L.P 5088, TANGA.

Barua pepe: cdmlingano@tari.go.tz

Mkonge ni zao linalostahimili sana ukame, magonjwa, na wadudu waharibifu. Hivyo mkonge unahitaji pembejeo chache kuliko mazao mengine katika uzalishaji. Mkonge hustawi kuanzia usawa wa bahari Mita 0 - 750 na kwenye maeneo yenye mvua kiasi cha Milimita 500 - 1200 kwa mwaka.

## AINA ZA MKONGE

Kuna aina nyingi za mkonge, lakini kwa sasa ni aina mbili tu ndizo zinazostawishwa kwa biashara nchini. Aina hizi ni mkonge wa asili unaojulikana kama *Agave sisalana* na mkonge chotara H. 11648.

## AINA ZA MICHE

1.**VIKONYO :** Hivi vijimimea vidogo hupatikana kwenye malingoti ya mkonge.

**2. MACHIPUKIZI**: Ni mimea ambayo huchipua kwenye mmea wa mkonge kuanzia mwaka mmoja na kuendelea.

3. **MICHE INAYOZALISHWA MAABARA:**

Ni mimea bora inayozalishwa maabara.



## UTAYARISHAJI WA KITALU

- Safisha vizuri na kuondoa visiki vyote
- Lima na kupiga rato "harrow" mpaka kupata udongo laini (fine tilth).
- Ondoa magugu yaliyoota kabla ya kupanda kwa kutumia harrow.
- Gawanya vitalu katika maboma madogo yenye eneo la robo hekta kila moja.Urefu mita 50 na upana mita 50.Hii itarahisisha utendaji kazi wakati wa kupanda na kuhudumia.

## JINSI YA KUPANDA

Nafasi za Kupanda Vikonyo

- Mbegu hupandwa Sm50 kati ya mistari na Sm 25 kati ya mimea.
- Kwa nafasi hii inakadiriwa kupata miche 80,000 kwa hekta moja/ekari 2.5.
- Ni vizuri vitalu vikapandwa juma moja au mawili kabla ya mvua. Vikonyo vinakuwa tayari kupelekwa shambani katika kipindi cha miezi12-18 tu.

**PALIZI:** Upaliliaji wa magugu unaweza kufanywa kwa njia mbili kuu yaani:-

1. Upaliliaji magugu kwa kutumia jembe la mkono
2. Uzuiaji magugu kwa kutumia madawa

## UPANDAJI WA MKONGE SHAMBANI

Uchaguzi na upandaji wa miche: Miche ya kupanda iwe na urefu kati ya Sm 50-70 na uzito kati ya kilo 2-4.

- Miche ipangwe katika madaraja kufuatana na

ukubwa.

## Utayarishaji wa miche

- Mizizi ikatwe bila kuharibu shina(bole), na majani yaliyonyauka yaondolewe.
- Miche ya mkonge ikishang'olewa ikae kwa muda wa majuma matatu bila kupandwa ili inyauke kidogo (Curing period).
- Maboma hupimwa (blocks) kwa kutumia mnyororo wa mita 50 kabla ya kupanda ili kutenganisha na kutoa nafasi ya barabara kwa ajili ya usafirishaji Mkonge.

Mifumo ya Upandaji Mkonge shambani.

## I.Mstari mmoja(Single row)

- Inapendekezwa kupanda kwa nafasi ya mita 3.86 kati ya miraba miwili na nafasi ya mita 0.86 kati ya mmea mmoja na mwingine
- Upandaji huu hutoa mimea 3012 kwa hekta.

**II. *Upandaji wa mistari miwili*** Nafasi ya Upandaji ni mita 4+1x1.miraba miwili huwekwa karibu ili kutoa nafasi pana kati ya miraba hiyo, nafasi kati ya mmea mmoja na mwingine ni mita moja. Upandaji huu hutoa mimea 4000 kwa hekta.

## Muda wa Kupanda

Inashauriwa kupanda mkonge kabla mvua hazijaanza, na mkonge upandwe kina cha sentimeta nane(8) ardhini na kushindiliwa, sehemu ambazo mkonge umekufa zirudishwe kati ya miezi 6 tangu kupandwa.

*Mbegu za Mkonge ambazo zipo tayari kupandwa shambani*



**UVUNAJI BORA WA ZAO LA MKONGE**

**(i) Mambo muhimu katika uvunaji wa majani ni:**

- Shamba liwe safi
- Jani liwe limekomaa
- Kata jani sehemu ya shingo,lisikatwe kitunguu au mapembe.
- Majani yaliyokatwa yafungwe katika mizigo ya majani 30 kila mzigo na kupanga meta ya mizigo 110.

**(ii) Usombaji wa majani yaliyokatwa :**

Ili kupata singa iliyo bora ni lazima majani yaliyokatwa yasombwe na kupelekwa kwenye korona mapema kabla ya siku tatu.

(iii) **Usindikaji na uanikaji wa singa:**

1. Majani yaliyokatwa ni lazima yasindikwe ndani ya saa 48
2. Baada ya kusindikwa singa (mshamo) ni lazima zitandazwe kwenye waya mara moja.
3. Kiwanja cha kuanikia ni lazima kifyekwe kwa mapanga au makwanja mara kwa mara. Ni marufuku kiwanja kuchomwa moto.
4. Singa (brush) ni lazima ianuliwe haraka mara tu inapothibitishwa kuwa imekauka.
5. Singa iliyoanuliwa iachwe ipoe kwa saa 12 kabla ya kulainisha kwenye kayamba.

**(iv) Kulainisha Singa:**

1. Singa ni lazima zilainishwe kwenye mashine/ kayamba.
2. Singa iliyolainishwa hupangwa kwenye masanduku au mizigo ya kilo 50.

**Kufunga Mizigo au Robota:**

1. Mizigo ya kilo 50 inafungwa kutoa robota. Hii inaweza kufanyika kwa mashine au kwa kufunga kawaida.

2. Wanunuzi wengine hupenda mizigo 5 ifungwe pamoja ili kupata robota la kilo 250 na wengine mizigo 4 pamoja ili kupata robota la kilo 200 na kadhalika.

3. Mizigo au robota lazima zipangwe juu ya mataruma au magogo ili yasinyonye unyevu (maji) kutoka kwenye sakafu.

4. Sehemu ya kuhifadhia robota au mizigo kuta na paa zake zisiwe zinavuja.

**(v) Kupanga madaraja ya Singa:**

Kuna madaraja mbali mbali ya singa. Madaraja ya singa hupangwa kulingana na rangi, urefu na usafi wa singa.

**Bidhaa Mbalimbali zitokanazo na Mkonge**

